AIMWA 010

# TOP MARK SERIES

## MUHULA WA TATU

## KISWAHILI LUGHA DARASA LA SITA

**Soma kifungu kifuatacho kisha uchague jibu sahihi**

Uchumi ___1___ tarafa ya Kiomo katika nchi jirani ___2___ ___3___ na ___4___ wa baada ___5___ uchanguzi mkuu wa taarafa ___6___ Bw. Raymond Mutua alisema ___7___ ya ___8___ 6,000 wa kampuni ya maua ___9___ vurungu za uchaguzi na ___10___ uhaba mkubwa. Aliongeza kuwa ___11___ cha chai ambacho ___12___ ___13___ majani chai kutoka kwa ___14___ wadogo wadogo kilichomwa. Bei ___15___ vyakula zimepanda.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A.wa | B. ya | C. za | D. la |
| 2. | A. umeathiriwa | B. umeadhirika | C. umeathirika | D. umeadhirika |
| 3. | A. sawa | B. uzuri | C. tena | D. vibaya |
| 4. | A. siasa | B. makabiliano | C. mtamauko | D. ukiwa |
| 5. | A. za | B. na | C. ya | D. kwa |
| 6. | A. hiyo | B. hilo | C. hio | D. huo |
| 7. | A. kwamba | B. zaidi | C. lakini | D. upungufu |
| 8. | A. wafanyikazi | B. wezi | C. wavamizi | D. wafanyikazi |
| 9. | A. wamekimbilia | B. wamekimbilia | C. wamekimbia | D. wamekimbia |
| 10. | A. kusababisha | B. kutoa | C. kupunguza | D. kuongeza |
| 11. | A. kampuni | B. kiwanda | C. makavazi | D. kichungi |
| 12. | A. kitakuwa | B. kitakua | C. kilikua | D.kilikuwa |
| 13. | A. kinapokea | B. kinapokeza | C. kinahudumia | D.kinapatia |
| 14. | A. wazazi | B. vizazi | C. wazalishaji | D. wazawa |
| 15. | A. ya | B. za | C. na | D. au |

**Kuanzia swali la 16-30 jibu kulingana na maagizo**

16. Msimu wa baridi kali huitwa?

A. vuli B. kipupwe
C. masika D. rasharasha

17. Kamilisha methali: Mtoto umleavyo ndivyo ____

A. akuwavyo B. akuavyo
C. akuwapo D. wakuapo


18. Mamaye mzazi wako wa kike utamwitaje?

A. Mama mkwe B. Babu
C. Nyanya D. Baba mkwe

19. Kijana mlafi alimeza ____ la ugali

A. doti B. tonge
C. biwi D. bunda

20. Hili ni umbo lipi?



A. Pembe nne B. Pembetatu
C. Mchinjo kati D. Humusi nne

21. $^4/_5$ hii ni akisami ipi?

A. Robo tano B. Humusi nne

C. Robo nne D. Humusi tano

22. Unda jina kutokana na kitenzi Amini

A. Mwamini B. Imani

C. Amini D. Muumini

23. Ni lipi pambo la sikioni?

A. Kikuku B. Kipuli

C. Kipini D. Kikuba

24. Mtoto ______ mchanga atunzwe

A. yeyote B. wowote

C. yoyote D. lolote

25. neno kalamu liko katika ngeli ya?

A. LI-YA B. A-WA

C. I-ZI D. I-I

26. Tumia enye

Chura ______ ameniuma

A. chenyewe B. yenye

C. mwenyewe D. mwenye

27. Ni neno lipi lisilofaa katika orodha hii

A. Runinga B. Rununu

C. Kinu D. Tarakilishi

28. **Kamilisha methali hii:** Paka hawekewi ______

A. asali kulinda B. wali kulinda

C. kitoweo kulinda D. moto

29. Kutokana na nomino mtego tunapata kitenzi kipi?

A. Tega B. Kutega

C. Mtegaji D. Tegatega

30. Chagua kivumishi sifa katika sentensi hii

Uzi mwembamba hukatika upesi?

A. Uzi B. Mwembamba

C. Hukatika D. Upesi

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31-40**

Sungura na Simba walikuwa marafiki wa chanda na pete. Siku moja Simba akamwambia Sungura, Yahe huna habari kuwa sasa tu watu wazima yatupasa tufanyeje ili tuyatengeneze maisha yetu? Sungura akajibu "mimi naona kuwa hatuna budi kuoa Simba alikubaliana na wazo hili na wote wakaoa.

Kila siku Simba alikwenda porini kuwinda wanyama naye akapendwa sana na mkewe. Sungura naye hakwenda kuwinda na mkewe alihuzunika mno kwa maana walikula majani kila siku. Siku moja aliamua kumuuliza mmewe Sungura sababu za kukosa kwenda mawindoni kama rafikiye Simba.

Sungura aliposikia maneno haya alikasirika sana akatwaa shoka, mkuki na gunia na kwenda zake porini. Baada ya kwenda mbali na kuchoka akawaona kanga wakila majani na akaenda karibu nao na akawaambia "ndugu zangu nikiwa katika gunia hili mnaweza kunichukua? Wale kanga wakasema hawawezi kumuinua nao pia wakamwomba Sungura awainue.

Sungura aliwaambia waingie kwenye gunia kisha akalifunga ili wasianguke. Aliwachukua moja kwa moja mpaka kwake. Kanga wale walipiga kelele mno. Sungura aliwaambia kuwa alikuwa akiwapeleka nyumbani na kuwatumia kama kitoweo. Walilia lakini wapi! Kilio si dawa. Aliwachukua moja kwa moja hadi nyumbani.Mkewe Sungura alifurahi sana na kupendezwa naye.

31. Ni nani aliyeanza mazungumzo?

A. Sungura B. Simba

C. Kanga D. Mkewe sungura

32. Semi iliyo na maana ya kuoa ni ______

A. kupata nyumba B. kupata mke

C. kupata jiko D. kupata mme

33. Kwa nini Sungura hakwenda kuwinda?

A. Alikuwa mvivu

B. Kukosa silaha

C. Hakupendelea nyama

D. Alitosheka kwa majani

34. Maneno ya mkewe sungura yalimfanyaje Sungura?

A. yalimkera B. yalimfurahisha

C. yalimridhisha D. alimchapa mkewe

35. Sungura alipokuwa akienda porini aliwaona kanga wakifanya nini majani?

A. Wakilala B. Wakila

C. Wakicheza D. Wakiimba

36. Kanga ni kiumbe gani?

A. Nyani B. Swara

C. Nyuni D. Mdudu

37. Sungura aliwatia kanga guniani kwa kutumia nini?

A. Mikuki B. Shoka

C. Mikono D. Ujanja

38. Kanga waliokuwa ndani ya gunia walikuwa wangapi?

A. Wengi B. Wachache

C. Wawili D. Mmoja

39. Methali inayoweza kutumiwa katika hadithi hii ni?

A. Umoja ni nguvu

B. Aliye juu mngoje chini

C. Mwenye nguvu mpishe

D. Akili ni mali

40. Kichwa mwafaka cha hadithi hii ni?

A. Simba na Sungura B. Sungura mjanja

C. Mkewe Sungura D. Kanga na Sungura

**<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41-50</u>**

Chawa ni mdudu mdogo akaaye mwilini wa binadamu hasa katika nywele na nguo chafu. Chawa hunyonya damu ya mwenyeji wake. Chawa wengi humsumbua binadamu sana kwa kumuumauma. Yeye naye hujaribu kuwatoa na kuwaua kwa kutumia vidole vyake. Kwa kawaida chawa ingawaje ni mdudu mdogo sana, hawezi kufa kwa kidole kimoja.

Mtu huwajibika kutumia vidole viwili kumfinya. Msemo huu kunyesha kwamba mtu akiwa peke yake hawezi kufanikiwa kutekeleza jambo lolote lile. Binadamu anahitaji msaada wa mwenziwe, kwani mtu ni watu.

41. Chawa huishi wapi?

A. Mwilini B. Popote

C. Kichwani D. Kitandani

42. Chawa hupenda kuishi kwa binadamu _______

A. safi B. asiyejali

C. mchafu D. anayejali

43. Chawa ______ damu ya mwenyeji wake

A. hula B. hunyonya

C. huvuta D. hufagia

44. Binadamu huwaua chawa kwa kutumai nini?

A. Meno yake B. Vidole vyake

C. Bunduki D. Kisu

45. Chawa hawezi kufa kwa vidole vingapi?

A. Vinne B. Sita

C. Kimoja D. Vitatu

46. Chawa ni _______

A. mnyama B. nzi

C. binadamu D. mdudu

47. Kulingana na hadithi kidole kimoja ______ chawa

A. hakiui B. huvunja

C. vua D. humaliza

48. Binadamu huhitaji ________

A. chawa B. mwenzake

C. kuumwa D. kusumbuliwa

49. Kulingana na hadithi mtu ni _______

A. wenzake B. chawa

C. watu D. binadamu

50. Hadithi hii inatufundisha kuwa ________

A. chawa ni mzuri

B. kuumwa ni kuzuri

C. mtu anahitaji watu